**MATUMIZI YA LUGHA**

**Kiimbo**

⇒ Jinsi sauti inavyopanda na kushuka mtu anapoongea.

⇒ Huibua maana halisi ya maneno yanayosemwa kama ifuatavyo:

- Sentensi za taarifa
- ✓ Mtoto anaandika barua.
- Sentensi za maswali
- ✓ Mtoto anaandika barua?
- Sentensi za mshangao
- ✓ Mtoto anaandika barua!
- Sentensi za amri
- ✓ Kachezeeni nje!
- Sentensi za rai/ombi
- ✓ Nisaidi**e/eni**.

**Zoezi**

a) Eleza maana ya kiimbo kwa kutoa mifano.

b) Tambua sentensi zifuatazo ni za aina gani kutokana na kiimbo.

i) Watu wanakula nyoka?

ii) Watu wanakula nyoka.

iii) Watu wanakula nyoka.

iv) Tafadhali nisaidie.

**Silabi**

⇒ Tamko moja katika neno/herufi moja au zaidi ambazo hutamkwa pamoja.

**Miundo Miwili ya Silabi za Kiswahili**

- **Silabi wazi**

⇒ Huishia kwa irabu k.m. o-**a**, (**I**) i-**ga** (KI), **mbu**-zi (KKI) na u-**ngwa** (KKKI)

- **Silabi funge**

  ⇒ Huishia kwa konsonanti k.m. **m**-tu (K)

**Zoezi**

a) Ukitoa mifano, fafanua miundo miwili ya silabi za Kiswahili.

b) Tenganisha silabi katika maneno yafuatayo:

  i) inkisari

  ii) baiskeli.

**Shadda/Mkazo**

⇒ Mkazo unaowekwa kwenye silabi fulani ya neno ikiwa imetamkwa kwa msisitizo.

⇒ Alama ya ritifaa hutumiwa kutambulisha shadda.

⇒ Huwekwa kwenye silabi ya pili kutoka ya mwisho, kwenye vitenzi vishirikishi vya silabi moja au kubadilisha maana ya neno.

✓ ka'lamu, I'mba, thu'mni, 'leta, n.k.

✓ Kitabu 'ki mezani.

✓ Bara'bara (njia), ba'rabara (sawasawa), wala'kini (lakini), wa'lakini (kasoro/dosari/ila)

**Zoezi**

a) Weka shada katika maneno haya:

i) imba

ii) baba

b) Onyesha kwa kupiga mstari iliko shada katika maneno yafuatayo:

i) malaika

ii) nge

**Sauti za Kiswahili**

⇒ Kuna makundi mawili ya sauti za kiswahili:

a) Irabu

⇒ Sauti ambazo hutamkwa kwa ulaini bila hewa kuzuiliwa katika ala za sauti.

b) Konsonanti

⇒ Sauti ambazo wakati wa kutamkwa hewa huzuiliwa katika ala za sauti.

- **Aina za Ala za Sauti**


a) Ala tuli

⇒ Ambazo hazisogei mtu akitamka k.m. meno, ufizi, kaa kaa gumu, kaa kaa laini na koo/koromeo.

b) Ala sogezi

⇒ Ambazo husogea mtu akitamka k.m. midomo na ulimi.

**Matamshi/Uainishaji wa Irabu**




a)

b) a ni ya katikati na chini kinywani na midomo ikiwa imeviringa.

c) e ni ya mbele na kati kinywani na midomo ikiwa imetandazwa.

d) i ni ya mbele na juu kinywani na midomo ikiwa imetandazwa.

e) o ni ya nyuma na kati kinywani na midomo ikiwa imeviringa.

f) u ni ya nyuma na juu kinywani na midomo ikiwa imeviringa.

**Zoezi**

a) Taja makundi mawili ya sauti za Kiswahili.

b) Yatofautishe makundi ya sauti za Kiswahili uliyotaja katika (a)

c) Toa mifano miwili miwili ya irabu ambazo hutamkwa:

  i) midomo ikiwa imeviringa

  ii) midomo ikiwa imetandazwa

d) Eleza jinsi irabu /e/ inavyotamkwa.

e) Taja aina mbili za ala za kutamkia na utoe mfano mfano mmoja mmoja.

**Matamshi/Uainishaji wa Konsonanti**

| MAHALI / AINA | MIDOMO | MDOMO MENO | MENO | UFIZI | KAAKAA GUMU | KAAKAA LAINI | KOROMEO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIPASUO (H)<br>(GH) | p<br>b | | | t<br>d | | k<br>g | |
| VIPASUO (GH)<br>KWAMIZO (H) | | | | | ch<br>j | | |
| NAZALI (GH)<br>(VING'ONG'O) | m | | | n | ny | ng' | |
| VIKWAMIZO (H)<br>(VIKWARUZO)(GH) | | f<br>v | th<br>dh | s<br>z | sh | gh | h |
| KITAMBAZA | | | | l | | | |
| KIMADENDE | | | | r | | | |
| NUSU IRABU<br>VIYEYUSHO | w | | | | y | | |

⇒ Huainishwa kulingana na inapotamkiwa, kuwepo au kutokuwepo kwa mtetemeko katika nyuzi za sauti na jinsi hewa inavyozuiliwa katika ala k.m. /p/ ni ya midomo, kipasuo na sighuna.

- **Vipasuo**

⇒ Konsonanti ambazo wakati wa kutamkwa hewa husukumwa, huzuiliwa kabisa na kuachiliwa kwa ghafla na mpasuko mdogo kutokea.

- **Vikwamizo/Vikwaruzo**

⇒ Konsonanti ambazo wakati wa kutamkwa hewa hupitishwa katikati ya ala kwa kukwamizwa.

- **Vipasuo kwamizo/kwaruzo**

⇒ Konsonanti ambayo wakati wa kutamkwa hewa husukumwa nje kwa nguvu, huzuiliwa kabisa halafu mwanya mdogo huachwa hewa ipite kwa kukwamizwa.

- **Nazali/Ving'ong'o**

⇒ Konsonanti ambazo wakati wa kutamkwa kuna kiasi cha hewa huachiliwa na kupitia puani

- **Kitambaza**

⇒ Konsonanti ambayo wakati wa kutamkwa hewa husukumwa kwa nguvu, kuzuiliwa na kuachiliwa ipite kando ya ulimi

- **Kimadende**

⇒ Konsonanti ambayo wakati wa kutamkwa hewa husukumwa, kuzuiliwa na kuachiliwa na kusababisha ncha ya ulimi kupigapiga ufizi mfululizo.

- **Nusu irabu/Viyeyusho**

⇒ Konsonanti ambazo wakati wa kutamkwa hewa hupitishwa katikati ya ala kwa ulaini kama katika utamkaji wa irabu.

**Zoezi**

a) Tambua kikwamizo cha kaakaa laini na kiyeyusho cha midomo.
b) Tambua konsonanti ambazo si za orodha hii na ueleze kwa nini: /m/, /n/, /ny/,/ng'/, /f/, /b/
c) Tofautisha konsonanti /p/ na /dh/.
d) Taja konsonanti mbilimbili ambazo hujulikana kama:
   i) viyeyusho
   ii) vikwaruzo

**Aina za Maneno**

**Nomino (N)**

⇒ Neno linalotaja kiumbe, kitu, hali, mahali, tendo, dhana, n.k.

**Aina**

- **Nomino za Pekee**

⇒ Ambazo hutaja kitu kwa kutumia jina lake/ambazo hutambulisha upekee wa kitu hicho.

⇒ Mwanzoni huandikwa kwa herufi kubwa.

✓ majina ya watu k.m. **K**amau
✓ mahali k.m. **M**ombasa
✓ siku k.m. **A**lhamisi
✓ miezi k.m. **D**isemba
✓ miaka k.m. 1930
✓ milima k.m. **K**ilimanjaro
✓ Mito k.m. **T**ana
✓ maziwa k.m. **V**ictoria
✓ bahari k.m. **H**indi
✓ Mabara k.m. **A**frica

- **Nomono za Kawaida/Jumla**

⇒ Majina ya jumla ya viumbe/vitu vinavyoonyesha umbile la jinsi moja k.m. mtu, gari, kalamu, n.k.

- **Nomino za Jamii**

⇒ Majina ya makundi ya viumbe au vitu k.m. bunge, jamii, halaiki, bunda n.k.

- **Nomino za Wingi**

⇒ Majina ya vitu vitokeavyo kwa wingi japo kimsingi hazina umoja au wingi k.m. maji, mate, maziwa, mahubiri, marashi, mchanga, ngeu, poda, unga, n.k.

- **Nomino za Dhahania**

⇒ Majina ya viumbe au mambo ya kudhani/yasiyoweza kugusika k.m. k.m ujinga, werevu, malaika, shetani, amani, imani, roho, wazo, dhana, n.k.

- **Nomino za Vitenzi Jina**

⇒ Vitenzi vyenye kiambishi awali **ku** ambavyo huweza pia kutumika kama nomino k.m. **Kucheza** kwake kunaudhi.

**Zoezi**

1. Sahihisha jedwali lifuatalo

| nomino | aina |
|---|---|

| | |
|---|---|
| Juma<br>kisu<br>maziwa<br>bunda<br>amani<br>kuomba | wingi<br>dhahania<br>pekee<br>kitenzi jina<br>kawaida/jumla<br>wingi |

2. Bainisha nomino katika sentensi ifuatayo

a) **Kuendesha baiskeli** kwa **kasi** kulimfanya **Hasani** aangushe **bunda** la noti alilokuwa anaenda kununulia **mchanga**.

**Sentensi ya Kiswahili**

⇒ Sentensi ni fungu la maneno linalojitosheleza kimaana linalotumiwa katika mawasiliano.

**Sifa**

a) Huwa na ujumbe uliokamilika.
b) Huwa na mpangilio maalum wa maneno.
c) Huwa na muundo wa kiima na kiarifu.

**Aina**

- **Sentensi Sahili**

⇒ Sentensi rahisi au nyepesi.

**Sifa**

a) Huwa fupi.
b) Huwa na kitenzi kimoja pekee.
c) Huwasilisha dhana moja.
d) Yaweza kuwa ya neno moja au zaidi.
e) Yaweza kuwa na kiima kilichododoshwa.

✓ Wataenda.
✓ Watoto wawili wanaelekea uwanjani.
✓ Gachiku ni msichana mtiifu.

- **Sentensi Ambatano**

⇒ Inayoundwa kwa kuunganisha sentensi sahili mbili.

**Sifa**

a) Huwa na vishazi huru viwili.
b) Huwa na kiunganishi.
c) Huwa na vitenzi viwili au zaidi.
d) Hutoa zaidi ya wazo moja.
e) Yaweza kuwa na viima vilivyododoshwa.

✓ Mwanafunzi alipita mtihani ingawa hakuwa anasoma kwa bidii.
✓ Maria aliendelea kupika kwa utaratibu huku akiimba wimbo.

- **Sentensi Changamano**

⇒ Ambayo huwa na kishazi tegemezi kilichochopekwa ndani.

**Sifa**

a) Huwa na kishazi tegemezi chenye kitenzi kinachovumisha nomino kwa kuirejelea.
b) Huwa na kishazi huru kimoja au zaidi.
c) Huwa na virejeshi (amba na O) au –enye.

✓ Tunda alilonunua jana limeoza.
✓ Mwizi aliiba pesa zilizokuwa kabatini.

**Kundi Nomino (KN) na Kundi Tenzi (KT)**

- Kundi Nomino ni sehemu katika sentensi inayoarifu kuhusu nomino na hutokea mwanzoni mwa sentensi.
- Kundi tenzi ni sehemu katika sentensi inayoarifu kuhusu kitenzi na hutokea mwishoni mwa

sentensi.

**Virai**

⇒ Vikundi vya maneno vitumiwavyo na binadamu visivyo na maana kamili.

⇒ Tungo zinayoundwa kwa maneno aghalabu mawili au zaidi yanayoashiria kitu kimoja na inayojengwa juu ya neno kuu.

**Aina**

- **Kirai Nomino (Kn)**
  a) W
  b) N
  c) N+U+N
  d) N+N+U+N
  e) N+$\overline{S}$
- **Kirai Kitenzi**
  a) T
  b) T+E
  c) T+N
  d) T+N+T
  e) TS+T
  f) t+N
  g) t+V+E
- **Kirai Kivumishi(Kv)**
  a) V+E
  b) V+U+V+E
  c) V+V+U+V+E
  d) V+N+V+E
- **Kirai kielezi (Ke)/Chagizo**
  a) E
  b) E+E
  c) E+E+E…
- **Kirai Kihusishi (Kh)**
  a) H+N
  b) H+N+V
  c) H+N+V+E

**Zoezi**

**Bainisha virai katika sentensi ifuatayo**

a) Mzazi na watoto wawili werevu sana waliwasili shuleni leo asubuhi kabla ya mwalimu.

**Vishazi**

⇒ Kundi la maneno lenye kiima na kiarifu likiwa ndani ya sentensi kuu.

**Aina**

- **Vishazi Huru**

⇒ Vifungu vya maneno katika sentensi ambavyo hutoa maana kamili.

- **Vishazi Tegemezi**

⇒ Vifungu vya maneno katika sentensi ambavyo havitoi maana kamili.

**Aina**

a) Vishazi tegemezi vya viunganishi k.m. Alimwadhibu **ingawa hakuwa na makosa**.
b) Vishazi tegemezi vya virejeshi k.m. Polisi walimpata mtoto **aliyekuwa amepotea**.

- **Vishazi Viambatani**

⇒ Vinavyoundwa kwa vishazi huru viwili vikiwa vimeunganishwa k.m. **Baba analala** na **mama anapika**.

**Zoezi**

**Bainisha Vishazi Katika Sentensi Zifuatazo**

a) Mwalimu amewasili.
b) Amina ambaye ni daktari atakuja.
c) Ametajirika japo hakupata elimu.
d) Mwalimu anafundisha na wanafunzi wanaandika.
e) Tumeanzisha shirika ili tunyanyue hali zetu.
f) Unaweza kuamua kunyamaza au kujitetea.

**Shamirisho/Yambwa**

**Aina**

- **Shamirisho Kipozi/Yambwa Tendwa**

⇒ Nomino inayoathiriwa na kitenzi.

- **Shamirisho Kitondo/Yambwa Tendewa**

⇒ Nomino inayotendewa kitendo.

- **Shamirisho Ala/Yambwa Kitumizi**

⇒ Chombo kinatumiwa kufanyia kitendo fulani.

**Mifano**

- ✓ Mama alimpikia **baba chakula** kwa **sufuria**.
- ✓ **Baba** alipikiwa **chakula** na mama kwa **sufuria**.
- ✓ **Sufuria** ilitumiwa na **mama** kumpikia **baba chakula**.

a) Chakula (Shamirisho Kipozi/Yambwa Tendwa)
b) Baba (Shamirisho Kitondo/Yambwa atendewa)
c) Sufuria (Shamirisho Ala/Yambwa Kitumizi)

**Ngeli za Nomino**

⇒ Makundi ya nomino katika lugha ya Kiswahili yenye sifa zinazofanana kisarufi.

- **A-WA**

⇒ Huwa na majina ya watu, vilema, viumbe, vyeo na viumbe vya kiroho, n.k.
⇒ Huchukua miundo kama vile M-WA, M-MI, KI-VI, n.k.

- ✓ mtu-watu,
- ✓ mkulima-wakulima
- ✓ mtume-mitume
- ✓ mkizi-mikizi
- ✓ kiwete-viwete
- ✓ kibyongo-vibyongo
- ✓ nabii-manabii
- ✓ kuku-kuku
- ✓ Waziri-Mawaziri

- **U-I**

⇒ Huwa na majina ya mimea, sehemu za mwili, vifaa, matendo, maumbile, n.k.
⇒ Huchukua muundo wa **M-MI**.

- ✓ Mchungwa-michungwa
- ✓ Mkoko-mikoko
- ✓ mkono-mikono
- ✓ mfupa-mifupa
- ✓ msumari-misumari
- ✓ mgomo-migomo
- ✓ mwendo-myendo
- ✓ msukosuko-misukosuko
- ✓ mlima-milima
- ✓ mwamba-myamba

- **U-YA**

⇒ Huwa na majina ya hali, matendo, n.k.
⇒ Huchukua muundo wa U-MA.

- ✓ Ugonjwa-magonjwa
- ✓ upana-mapana
- ✓ uasi-maasi
- ✓ uchungu-machungu
- ✓ ulezi-malezi
- ✓ uovu-maovu
- ✓ uhusiano-mahusiano

- **YA-YA**

⇒ Huchukua muundo wa MA-MA.
⇒ Huwa na nomino zipatikanazo kwa wingi.
⇒ Hazibadiliki katika umoja na wingi.

- ✓ manukato
- ✓ mauti
- ✓ maziwa
- ✓ marashi
- ✓ mahubiri
- ✓ majira
- ✓ maradhi
- ✓ maafa
- ✓ mazingira

- **KI-VI**

⇒ Ni majina ya vifaa, sehemu za mwili, vitu, udogo, lugha, n.k.
⇒ Huchukua miundo KI-VI na CH-VY.

- ✓ kisu-visu
- ✓ kitabu-vitabu
- ✓ chakula-vyakula
- ✓ chanda-vyanda
- ✓ kijitu-vijitu
- ✓ kigombe-vigombe
- ✓ kiguu-viguu
- ✓ kidovu-vidovu

- **LI-YA**

⇒ Huwa na majina ya sehemu za mwili, dhana, vifaa, ukubwa, n.k.

⇒ Huchukua muundo wa JI-MA, JI-ME, JA-MA, JE-MA n.k.

- ✓ jicho-macho
- ✓ jina-majina
- ✓ jitu-majitu
- ✓ goma-magoma
- ✓ jambo-mambo
- ✓ janga-majanga
- ✓ jembe-majembe
- ✓ jeneza-majeneza
- ✓ wazo-mawazo
- ✓ tunda-matunda
- ✓ jua-majua
- ✓ ziwa-maziwa
- ✓ ua-maua

▪ **I-I**

⇒ Huwa na nomino dhahania na vitu visivyoweza kuhesabika.

⇒ Hazibadiliki katika umoja na wingi.

- ✓ sukari
- ✓ amani
- ✓ chai
- ✓ mvua
- ✓ Imani
- ✓ chumvi
- ✓ subira
- ✓ imani
- ✓ amani
- ✓ furaha

▪ **I-ZI**

⇒ Huhusisha nomino dhahania na vitu.

⇒ Hazibadiliki katika umoja na wingi.

- ✓ nyumba
- ✓ baiskeli
- ✓ karatasi
- ✓ redio
- ✓ meza
- ✓ dini
- ✓ dawa
- ✓ ndizi
- ✓ jozi

▪ **U-ZI**

⇒ Huchukua miundo W-NY, U-NY, U-F, n.k.

- ✓ wayo-nyayo
- ✓ wakati-nyakati
- ✓ uso-nyuso
- ✓ ufa-nyufa
- ✓ ufunguo-funguo
- ✓ ufagio-fagio
- ✓ wembe-nyembe
- ✓ uwanja-nyanja
- ✓ ujumbe-jumbe
- ✓ ukoo-koo
- ✓ waraka-nyaraka
- ✓ waya-nyaya

▪ **U-U**

⇒ Huwa na nomino za dhahania na vitu visivyoweza kuhesabika.

⇒ Hazibadiliki kimaumbo.

- ✓ Huchukua U au W.
- ✓ Ujinga
- ✓ Ulafi
- ✓ Ulaji
- ✓ Werevu
- ✓ Unga
- ✓ Uji
- ✓ Ugali
- ✓ udongo

▪ **KU**

⇒ Nomino zinazoundwa kutokana na vitenzi k.m. **kuomba** kwake kumemsaidia.

▪ **PAKUMU**

⇒ Ngeli ya mahali.

⇒ Huwa na nomino moja 'mahali'.

a) PA (mahali karibu au panapodhihirika) k.m. Kitabu ki**po pa**le.
b) KU (mahali mbali au kusikodhihirika) k.m. Mahali **ku**le **ku**nafaa.
c) MU (ndani ya) k.m. Mahali **m**le **m**na siafu.

**Zoezi**

a) Tunga sentensi ukitumia nomino kutoka katika ngeli ya U-ZI.
b) Andika kwa wingi. Makaribisho aliyopewa yalimfurahisha.

c) Andika katika ukubwa wingi: Paka mweupe amenaswa mguuni.
d) Andika katika wingi wa hali ya udogo: Mtu aliumwa na mbwa.
e) Huku ukitoa mifano, fafanua miundo mitatu ya majina katika ngeli ya LI-YA.
f) Tambua ngeli/viwakilishi ngeli vya nomino zifuatazo:
   i) chakula
   ii) shairi
   iii) mtwana

**Uundaji wa maneno**

- **Nomino kutokana na mzizi wa kitenzi**

a) danganya-kudanganya, mdanganyifu,udanganyifu
b) soma-kusoma, masomo,msomi,usomaji
a) mlo-kula
b) mlevi-kulewa, kulevuka
c) mwimbaji-kuimba

- **Nomino kutokana na mzizi wa nomino**

a) mwimbaji-kuimba, wimbo, uimbaji, kiimbo
b) mchezo-kucheza, uchezaji, mchezaji
c) ulaghai-kulaghai, mlaghai
d) hesabu-kuhesabu,uhesabu
e) mdhalimu- kudhulumu, dhuluma, udhalimu
c) unda-kuunda, muundaji,uundaji,muundo
d) funika-kufunika, kifuniko, mfunikaji, ufunikaji

- **Kitenzi kutokana na mzizi wa nomino**

d) fikra-kufikiri
e) malezi-kulea
f) fumbo-kufumba, kufumbua

- **Nomino kutokana na mzizi wa kivumishi**

a) -refu-mrefu, urefu, urefushaji
b) -baya-mbaya, ubaya
c) -zuri-mzuri, uzuri
d) -kali-mkali, ukali
e) -eupe-mweupe,weupe

- **Kivumishi kutokana na mzizi wa nomino**

a) ujinga -jinga
b) werevu -erevu
c) mzuri -zuri
d) mpumbavu -pumbavu
e) mpyoro -pyoro

- **Kitenzi kutokana na mzizi wa kivumishi**

a) haramu-kuharamisha, kuharamika
b) halali-kuhalalisha, kuhalalika
c) -fupi-kufupisha, kufupika
d) bora-kuboresha, kuboreka
e) -refu-kurefusha, kurefuka
f) sahihi-kusahihisha, kusahihika
g) -sikivu-kusikia
h) -danganyifu-kudanganya

- **Kivumishi kutokana na mzizi wa kitenzi**

a) dunisha - duni
b) Haramisha - haramu
c) fupisha -fupi
d) sahilisha -sahili
e) tukuka -tukufu
f) fahamu -fahamivu
g) teua -teule
h) nyamaza -nyamavu
i) ongoka -ongofu
j) sahihisha -sahihi
k) danganya -danganyifu

- **Kitenzi kutokana na kielezi**

a) haraka-harakisha
b) zaidi-zidisha
c) bidii-bidiisha
d) hima-himiza

**Zoezi**

a) Unda neno ulilopewa katika mabano kutokana na maneno yafuatayo:
   i) zingatia (kivumishi)
   ii) sahili (kitenzi)
   iii) taliki (nomino)
b) Unda nomino kutokana na mizizi ya maneno yafuatayo kisha utunge sentensi.
   i) -kali
   ii) lia

**Vitenzi**

⇒ Kitenzi ni neno linaloeleza kuhusu jambo linalofanywa.

**Aina za Vitenzi**

- **Kitenzi halisi**

⇒ Kinachofahamisha tendo halisi.
⇒ Hutokea peke yake k.m. Boke **anacheza** mpira.

- **Kitenzi kikuu (T)**

⇒ Kinachoeleza tendo kuu katika sentensi.
⇒ Hutokea pamoja na kitenzi kisaidizi k.m. Baba anataka **kulala**.

- **Kitenzi Kisaidizi (Ts)**

⇒ Kinachosaidia kitenzi kikuu

**Maneno yanayoweza kutumiwa kama vitenzi visaidizi**

✓ ngali
✓ kuwa
✓ taka
✓ pasa
✓ bidi
✓ huenda
✓ kuja
✓ weza
✓ kwisha
✓ stahili
✓ wahi
✓ maliza

- **Vitenzi Sambamba**

⇒ Vinavyofuatana moja kwa moja/vinavyotokea kwa mfululizo.
⇒ Hutumika kutoa maelezo kuhusu tendo moja maalum kwa uwazi zaidi.
✓ Wachezaji **huenda wanaweza kushinda** mchezo wa leo.

- **Vitenzi Vishirikishi (t)**

⇒ Vinavyoshirikisha vitu kihali, kitabia au kimazingira.

**Aina**

a) **Vitenzi Vishirikishi Vikamilifu**

⇒ Ambavyo huchukua viambishi.

✓ Mama **alikuwa** mgonjwa/jikoni/muuguzi.

✓ Aisha **angali** kitandani/mkaidi/ mwanafunzi.

b) **Vitenzi Vishirikishi Vipunguvu**

⇒ Ambavyo havichukui viambishi

| kuyakinisha | kukanusha |
|---|---|
| **ni**/niko<br>**ndi**ko<br>**yu**ko<br>**li**/liko | si/siko<br>siko<br>hayuko<br>hali/haliko |

**Viwakilishi (W) na Vivumishi (V)**

☝ Viwakilishi ni viambishi au maneno yanayotumiwa badala ya nomino.

☝ Vivumishi ni maneno yanayotoa habari zaidi kuhusu nomino.

<table>
<tr><td>VIVUMISHI</td><td>VIWAKILISHI</td></tr>
<tr><td>Viulizi</td><td>Viulizi</td></tr>
<tr><td>☝ Maneno ya kuulizia.<br>☝ Mizizi ni –pi, -ngapi na gani.<br>✓ Amechukua kitabu kipi?(V. kiulizi)</td><td>✓ Kipi kimepotea? (W. Kiulizi)<br>✓ Amenunuliwa mangapi?<br>✓ Gani imefungwa?</td></tr>
<tr><td>a-unganifu</td><td>a-unganifu</td></tr>
<tr><td>☝ Maneno yanayoundwa kwa viwakilishi ngeli na kiishio a.<br>☝ Hutoa maana ya umilikaji<br>✓ Mtoto wa shangazi amelala. (V. a-unganifu)</td><td>✓ Wa Juma analia. (W. a-unganifu)<br>✓ Cha mlevi huliwa na mgema.</td></tr>
<tr><td>Vimilikishi</td><td>Vimilikishi</td></tr>
<tr><td>☝ Hutoa maana ya umilikaji.<br>Mizizi
<table>
<tr><td>nafsi</td><td>kuyakinisha</td><td>kukanusha</td></tr>
<tr><td>1<br>2<br>3</td><td>-angu<br>-ako<br>-ake</td><td>-etu<br>-enu<br>-ao</td></tr>
</table>
✓ Kiatu changu kimepotea. (V. kimilikishi).</td><td>✓ Usichukue chake. (W. kimilikishi)</td></tr>
<tr><td>Sifa</td><td>Sifa</td></tr>
<tr><td>☝ Maneno ya kusifu au kueleza jinsi nomino ilivyo k.m. -fupi, -baya, -kali, -dogo, n.k.<br>✓ Mti mrefu umeanguka. (V. sifa)</td><td>✓ Alichukua cheupe. (W. Sifa)</td></tr>
<tr><td>Vionyeshi/viashiria</td><td>Vionyeshi/viashiria</td></tr>
<tr><td>☝ Maneno ya kuonyesha nomino ilipo.<br>☝ Huwa za karibu, wastani na mbali k.m. hili, hilo, lile.<br>✓ Kiatu hiki kimechafuka. (V. kionyeshi/kiashiria)</td><td>Hii ni ya nani? (W. kionyeshi/kiashiria)</td></tr>
<tr><td>Viashiria visisitizi</td><td>Viashiria visisitizi</td></tr>
</table>

| | |
|---|---|
| ☝ Maneno ya kutilia mkazo nomino yakizingatia ilipo.<br>☝ Huwa ya karibu, wastani na mbali.<br>☝ Huundwa kwa kutumia kiwakilishi ngeli katika kionyeshi cha kwanza k.m. **ki**ki hiki -**vi**vi-hivi, lili hili-**ya**ya haya, n.k.<br>✓ Chumvi **ii hii** ilimwagika. (**V. kisisitizi**) | ✓ **Kuku huku** ndiko kulinyesha. (**W. kisisitizi**) |
| **Virejeshi** | **Virejeshi** |
| ☝ Hurejelea nomino au kukumbusha kuihusu.<br>☝ Huwa amba- na -o- rejeshi.<br>✓ Mtoto **ambaye** analala ni wake.<br>✓ Watoto wana**o**lala ni wao. (V. kirejeshi)<br>✓ Mnyama **ambaye hu**windwa ni nguruwe.<br>✓ Mnyama awindwa**ye** ni nguruwe. | ✓ **Amba**ye aliniibia ninamjua.<br>✓ Ali**ye**niibia ninamjua.<br>✓ **Amba**ye hula nyasi ni ng'ombe.<br>✓ Ala**ye** nyasi ni ng'ombe. |
| **Idadi** | **idadi** |
| ☝ Hutaja idadi ya nomino<br>**Aina**<br>a) **Idadi halisi** (iliyo dhahiri) k.m. -moja, sita, n.k.<br>b) **Idadi ya jumla (**isiyo dhahiri) k.m. -chache, -kadha –ingi, n.k.<br>✓ Mwalimu **mmoja** na wanafunzi **sita** wameenda. (**V-idadi halisi**)<br>✓ Vitabu **vichache** vimechukuliwa na watoto **kadha**. (**V. idadi ya jumla**) | ✓ Nipe **kumi na kimoja**. (**V. idadi halisi**).<br>✓ Amechukua **machache** tu. (**V. idadi ya jumla**) |
| **Pekee** | **Pekee** |
| ☝ Hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino kwa njia ya pekee.<br>a) –**enye** (u**milikaji)**<br>✓ Msichana **mwenye** maringo ni yule. (**V. Pekee**)<br>b) –**enyewe** (h**alisi** au **kusisitiza)**<br>✓ Barua **yenyewe** niliipeleka posta.<br>c) –**ote** (**bila kubakisha)**<br>✓ Chakula **chote** kimeliwa.<br>d) **-o-ote (bila kubagua)**<br>Mtu **yeyote** anaweza kuugua.<br>e) **-ingine** (s**ehemu ya baadhi ya vitu)**<br>✓ Mikufu **mingine** imeibwa.<br>f) -ingine-o (m**bali na/zaidi ya)**<br>✓ Nyuzi **nyinginezo** zilikatika. | ✓ **Mwenye** macho haambiwi tazama. (**W.pekee**)<br>✓ **Yenyewe** yaliiva jana.<br>✓ Kiliharibika **chote**.<br>✓ **Popote** paliposafishwa pamechafuka.<br>✓ Ametorokea **kwingine**.<br>✓ **Nyingineyo** niliweka katika chakula. |
| **Nomino/majina** | ⌖ |
| ⇒ Nomino/majina ambayo hutumika kama vivumishi<br>✓ Mtu **mzee** hutembea kwa mkongojo. (**V. jina/nomino**) | |
| ⌖ | **Ngeli** |

<table>
<tr><td></td><td>Viwakilishi ngeli ambavyo huwakilisha nomino k.m. Liliiva jana-Yaliiva jana.</td></tr>
<tr><td>⌖</td><td>Nafsi</td></tr>
<tr><td></td><td>⇒ Maneno au viambishi vinavyotajia nafsi.<br>Aina<br>a) Nafsi huru<br>⇒ Maneno ya kutajia nafsi.
<table>
<tr><th>nafsi</th><th>umoja</th><th>wingi</th></tr>
<tr><td>1</td><td>Mimi</td><td>Sisi</td></tr>
<tr><td>2</td><td>Wewe</td><td>Nyinyi</td></tr>
<tr><td>3</td><td>yeye</td><td>wao</td></tr>
</table>
✓ Yeye ni mtiifu. (W. nafsi huru)<br>b) Nafsi tegemezi/viambata<br>⇒ Viambishi ambavyo hutaja nafsi.
<table>
<tr><th>nafsi</th><th>umoja</th><th>wingi</th></tr>
<tr><td>1</td><td>ni</td><td>tu</td></tr>
<tr><td>2</td><td>u</td><td>m</td></tr>
<tr><td>3</td><td>a</td><td>wa</td></tr>
</table>
✓ Walisahau kumwambia. (W. nafsi tegemezi)</td></tr>
</table>

**Vielezi (E)**

⇒ Viambishi au maneno yanayoeleza zaidi kuhusu kivumishi, kitenzi au kielezi kingine.

✓ Yeye ni mweupe **sana/ajabu/kwelikweli/kupindukia/pepepe**.

✓ Alikula **pole pole sana**.

**Aina**

a) **Vielezi vya Namna/Jinsi**

⇒ Ambavyo hueleza **vile** jambo lilifanyika.

**Aina**

- **Vielezi namna mfanano**

⇒ Vinavyoeleza vile jambo lilifanyika kwa kufananisha na nomino au vivumishi.

⇒ Huchukua viambishi **KI** na **VI**.

✓ Anakula **ki**fisi.

✓ Tulifanya kazi **vi**zuri.

- **Vielezi namna viigizi**

⇒ Maneno ambayo kiasili ni vielezi k.m. sana, haraka, ghafla, mno, kabisa, pole, barabara n.k.

✓ Mwenda **pole** hajikwai.

- **Vielezi namna hali**

⇒ Hueleza hali ya tendo.

✓ Alilelewa **kwa shida**.

✓ Alilewa **chakari**

- **Vielezi namna vikariri**

⇒ Huelezea vile jambo lilifanyika kwa kurudiwarudiwa

✓ Alinijibu **kimzahamzaha.**

- ✓ Tembea **polepole.**
- ✓ Yeye hufanya kazi yake **hivi hivi/ovyo ovyo**
- ✓ Mbwa alibweka **bwe! Bwe! Bwe**!
- ▪ **Vielezi namna ala**
- ✓ Walimpiga Stephano **mawe/kwa mawe.**
- ▪ **Vielezi Namna Viigizi**
- ⇒ Hueleza vile kitendo kilitendeka kwa kutumia tanakali.
- ✓ Mbuni alianguka majini **chubwi!**

b) **Vielezi vya Idadi/Kiasi**

⇒ Maneno ambayo hutaja kitendo kimetendeka mara ngapi.

**Aina**

- ▪ **Vielezi vya idadi halisi**
- ✓ Tulivamiwa **mara moja.**
- ▪ **Vielezi vya idadi ya jumla**
- ✓ Alitoroka **mara kadha/nyingi/chache.**

**c) Vielezi vya mahali**

⇒ Hutaja mahali kitendo kilitendekea.

**Aina**

- ▪ **Vielezi vya mahali vya maneno kamili**
- ✓ Ndege ilipofika **Nairobi**, ilitua **chini**.
- ▪ **Vielezi vya mahali vya aina ya viambishi**
- ⇒ Ni viambishi **po, ko, mo na ni.**
- ✓ Ali**po**lala palikuwa na siafu.
- ✓ Wanacheza uwanja**ni.**

**d) Vielezi vya wakati**

⇒ Hutaja kitendo kililifanyika wakati gani**.**

**Aina**

- ▪ **Vielezi vya wakati vya maneno kamili**
  - ✓ Rais atawasili **kesho/mwaka ujao.**
- ▪ **Kielezi cha wakati cha kiambishi (po** ya wakati)
  - ✓ Nililala nili**po**fika nyumbani

**Viunganishi (U)**

⇒ Neno au fungu la maneno la kuunganishia.

**Aina**

- ▪ **Vya kujumuisha pamoja**
- ✓ na
- ✓ aidha (pia)
- ✓ isitoshe
- ✓ kadhalika (pia))
- ✓ tena
- ✓ mbali na
- ✓ fauka ya (zaidi ya)
- ▪ **Vya kukatiza ili kupambanua**
- ✓ walakini (lakini)
- ✓ bali (lakini)
- ✓ ijapokuwa (hata kama)
- ✓ ingawa (hata kama)
- ▪ **Vya kuonyesha kinyume cha mambo**
- ✓ ilhali
- ✓ licha ya
- ▪ **Kuonyesha masharti**
- ✓ budi (lazima)
- ✓ lazima
- ✓ sharti
- ✓ ikiwa (kama)
- ✓ bidi
- ▪ **Vya sababu**
- ✓ kwa
- ✓ kwa sababu
- ✓ maadamu (kwa kuwa)
- ✓ madhali (kwa kuwa)
- ✓ kwa vile/maana
- ✓ kwa ajili/minajili ya
- ✓ mintaarafu (kutokana na)
- ▪ **Vya kuonyesha Chaguo**
- ✓ au
- ✓ ama
- ✓ wala

- **Viunganishi vingine na maana zake**
- ✓ ila (isipokuwa)
- ✓ laiti (kama)
- ✓ lau (kama)
- ✓ mradi (bora)
- ✓ angalau (bora zaidi)
- ✓ bighairi (bila ya kujali) k.m.**Minghairi** vitu vilivyo kwenye kabati vinginevyo unaweza kuvichukua.
- ✓ seuze/sembuse (kulinganisha ili kuonyesha tofauti)
- ✓ labda (pengine)

**Vihusishi (H)**

⇒ Maneno yanayoonyesha uhusiano.

**Aina**

- **Mahali**
- ✓ juu ya, miongoni mwa, katika, mpaka, hadi
- **Wakati**
- ✓ kabla ya, baada ya, tangu, hadi, mpaka
- **Sababu**
- ✓ kwa, kwani, kwa sababu, mintaarafu ya
- **Ala**
- ✓ Alimkata **kwa** kisu.
- **A-unganifu**
- ✓ Simu **ya** rununu inalia.
- ✓ Jumba **la** mikutano limeandaliwa.
- ✓ Kiatu **cha** ngozi hudumu.
- ✓ Kikome **cha** plastiki ni duni.
- **Ulinganisho**
- ✓ Zaidi ya, kuliko, kuzidi, kushinda.
- **Kiwango**
- ✓ Zaidi ya, kati ya, takriban, karibu
- **Vya hali**
- ✓ Mithili ya, kwa niaba ya

**Vihisishi (I)**

⇒ Maneno yanayotoa hisia za moyoni.

a) furaha
- ✓ Hoyee! Haleluya! Alhamdulilahi!

b) hasira
- ✓ Kefle! Ah! He!

c) majuto
- ✓ Kumbe! Jamani! Ole wangu! Laiti

d) huzuni/huruma
- ✓ Pole! Ole! Maskini!

e) kuitikia
- ✓ Bee! Labela! Naam! Ehee! Ahaa!

f) mshangao/mshtuko
- ✓ Eti! Salaale! Ajabu! Msalia mtume! Lahaula!

g) kubeza
- ✓ Mawe! Ngo! Mmm! Mwangalie!

h) kusisitiza
- ✓ Hata

i) kutakia heri
- ✓ inshallah

Mwingiliano wa Maneno

⇒ Hali ya maneno kuwa na matumizi tofauti mifano:

- **W kuwa V**
- ✓ **Huyu** analia.
- ✓ Mtoto **huyu** analia.
- **V kuwa W**
- ✓ Vikombe **vizur**i vitavunjika.
- ✓ **Vizuri** vitaliwa.
- **V kuwa N**
- ✓ Mti **mrefu** haupandiki.
- ✓ **Mrefu** alikufa jana jioni.
- **V kuwa E**
- ✓ Viatu **vibaya** vitachomwa.
- ✓ Uliifanya kazi **vibaya.**
- ✓ Mtu **mjinga** ni huyu.
- ✓ Anaongea **kijinga.**
- **N kuwa V**
- ✓ **Tajiri** alimdharau Razaro.
- ✓ Mtu **tajiri** huheshimiwa.
- **N kuwa E**
- ✓ **Nairobi** ni mji mkuu.
- ✓ Amewasili **Nairobi.**
- ✓ **Kitoto** kinalia.
- ✓ Unaongea **kitoto.**
- ✓ **Haraka** haina baraka.
- ✓ Fanya **haraka** tuondoke hapa.
- ✓ **Sindano** ya babu imepotea
- ✓ Alidungwa **sindano/kwa sindano** na daktari.
- **E kuwa N**
- ✓ Niliwasili **jana**.
- ✓ **Jana** yangu haikuwa nzuri.
- **T kuwa N**
- ✓ Nataka **kulala** sasa.
- ✓ **Kulala** kwake kunaudhi.
- **N kuwa U**
- ✓ **Ila** yake imemwathiri sana.
- ✓ Watu wote **ila** yeye walikwenda.

- ✓ Kichwa changu kina **walakini**.
- ✓ Nimekula **walakini** sijashiba.
- ▪ **E kuwa I**
- ✓ Mwenda **pole** hajikwai.
- ✓ **Pole!** Usijali utapona.
- ✓ Amepaka rangi **sawasawa**.
- ✓ **Sawasawa**! Siku moja tutakutana.
- ▪ **H kuwa E**
- ✓ Paka amepanda **juu ya mti**.
- ✓ Ameingia **katika choo**.
- ▪ **T kuwa E**
- ✓ Mtoto **akilia** atatapika.
- ✓ Aliingia **akilia**.
- ▪ **N kuwa I**
- ✓ Gege anacheza **ala** yake ya muziki.
- ✓ **Ala!** Waniwekea uchafu katika chakula?

**Mofimu**

⇒ Kipashio kidogo zaidi katika lugha kisichoweza kuvunjwavunjwa zaidi bila kupoteza maana yake.

**Aina**

- ▪ **Mofimu huru**

⇒ Neno lisiloweza kugawanywa katika vipande mbalimbali na linalojisimamia na kuwa na maana kamili.

- ✓ Kuku, baba, mama, sana, labda, jana n.k.
- ▪ **Mofimu tegemezi**

⇒ Isiyoweza kujisimamia na kujitosheleza kisarufi, mifano:

- ▪ **Mzizi** (Sehemu ya neno inayobeba maana kuu na isiyoweza kubadilishwa)
- ✓ **m-tu, samahe-**k-a, n.k.
- ▪ **Nafsi**
- ✓ **Tu**mesahau
- ▪ **Ngeli**
- ✓ **Li**lianguka.
- ✓ **Ya**lianguka.
- ▪ **Kikanushi**
- ✓ **Si**kumpiga
- ✓ **Ha**lijaoza.
- ✓ **Hu**li.
- ▪ **Njeo/wakati**
- ✓ Li**li**iva.
- ✓ A**na**lia.
- ✓ Tu**ta**imba.
- ✓ Ali**po**enda.
- ▪ **Hali**
- ✓ **Me, nge, ngali, hu, ki, ka, n.k.**
- ▪ **Mahali**
- ✓ Ali**po**ingia.
- ✓ Ali**ko**ingia.
- ✓ Ali**mo**ingia.
- ▪ **Virejeshi**
- ✓ Lili**lo**nunuliwa.
- ✓ Ali**ji**kata.
- ▪ **Mtendwa/watendwa/kitendwa/vitendwa/shamirisho**
- ✓ Alichi**ki**chukua.
- ✓ Kilicho**wa**ua.
- ▪ **Mnyambuliko/kauli**
- ✓ Alimpig**i**a.
- ✓ Aliml**i**l**i**a
- ✓ Alinikos**e**a.
- ✓ Alimto**le**a.
- ▪ **Kiishio**
- ✓ a, e, i, u

**Viambishi**

⇒ Viungo vyenye maana vinavyofungamanishwa na mziziwa neno ili kulipa maana mbalimbali.

**Aina**

- ▪ **Viambishi Awali**

⇒ **Ambavyo** hutokea kabla ya mzizi.

- ✓ **A-li-ye-ku-**kata-a
- ▪ **Viambishi Tamati**

⇒ Ambavyo hutokea baada ya mzizi k.m. ki-pig**-ishw-a-cho**

**Mnyambuliko wa Vitenzi**

⇒ Kunyambua kitenzi ni kukiongeza viambishi tamati ili kukipa maana tofauti.

**Aina za minyambuliko/kauli za vitenzi**

- ▪ **Kutenda**

⇒ Hali ya kawaida ya kitenzi.

- **Kutendatenda**

⇒ Hali ya kitenzi kurudiwa.

- **Kutendea**

✓ Kwa niaba ya
✓ Badala ya
✓ Sababu
✓ Kuonyesha kitumizi
✓ Mwendo wa kitu kuelekea kingine

- **Kutendwa**

⇒ Huonyesha nomino iliyoathiriwa na kitenzi.

- **Kutendewa**

⇒ Humaanisha kitendo kimetendwa na mtu badala au kwa niaba ya mtu mwingine.

- **Kutendana**

⇒ Unamtenda mtu jambo naye anakutenda jambo lilo hilo.

- **Kutendeana**

⇒ Unamtendea mtu jambo naye anakutendea jambo lilo hilo.

- **Kutendeka**

⇒ Uwezekano wa kitendo kufanyika

- **Kutendesha**

⇒ Mtu au kitu kusababisha kufanyika kwa kitendo.

- **Kutendeshea**

⇒ Kusababisha kitendo kitendeke kwa niaba ya mwingine.

- **Kutendeshwa**

⇒ Kusababishwa kufanya jambo.

- **Kutendeshewa**

⇒ Mtu kusababishwa kitendo kitendeke kwa niaba yake.

- **Kutendeshana**

⇒ Kusababisha kitendo kitendeke kwa mtu naye anasababisha kitendo kicho hicho kitendeke kwako.

- **Kutendesheana**

⇒ Kusababisha kitendo kitendeke kwa niaba ya mtu naye anasababisha kitendo kicho hicho kitendeke kwa niaba yako.

- **Kutendesheka**

⇒ Kitendo fulani kinaweza kusaababishwa.

- **Kutendama**

⇒ Kuwa katika hali fulani bila ya mabadiliko.

✓ lala-lalama
✓ ficha-fichama
✓ shika-shikama
✓ ganda-gandama
✓ chuta-chutama
✓ funga-fungama
✓ kwaa-kwama
✓ unga-ungama
✓ andaa-andama
✓ saki-sakama

- **Kutendata**

⇒ Hali ya mgusano au kushikanisha vitu viwili.

✓ paka-pakata
✓ fumba-fumbata
✓ kokoa-kokota
✓ okoa-okota
✓ kama-kamata

- **Kutendua**

⇒ Hali ya kiyume

✓ choma-chom**o**a

- ✓ fung**u**a
- ▪ **Kutenduka**

⇒ Kuweza kufanyika kwa hali ya kinyume.
- ✓ chom**ok**a
- ✓ fung**uk**a

**Vinyume vya vitenzi**
- ✓ komea-komoa
- ✓ bariki-laani
- ✓ patana-kosana
- ✓ angika-angua
- ✓ mwaga-zoa
- ✓ ziba-zibua
- ✓ tatiza-tatua
- ✓ funika-funua
- ✓ tega-tegua
- ✓ tawanya-kusanya
- ✓ ugua-pona
- ✓ nasa-nasua
- ✓ kwamiza-kwamua
- ✓ kosa-kosoa
- ✓ pakia-pakua
- ✓ twika-tua
- ✓ paa-tua
- ✓ cheka-lia
- ✓ anika-anua
- ✓ simama-keti
- ✓ fukia-fukua
- ✓ inama-inuka
- ✓ funga-fungua
- ✓ furahi-huzunika
- ✓ kumbuka-sahau
- ✓ oa-taliki
- ✓ choka-pumzika
- ✓ uliza- jibu
- ✓ jenga-bomoa
- ✓ ishi-kufa/hama
- ✓ kufa-kufufuka/ishi
- ✓ lewa-levuka
- ✓ anza-maliza/isha
- ✓ saza/bakiza-maliza
- ✓ meza-tapika/tema
- ✓ ingia-toka
- ✓ dharau-heshimu
- ✓ kweya-teremka
- ✓ panda-shuka
- ✓ sifu-kashifu
- ✓ chimba-fukia
- ✓ chafua-safisha
- ✓ cheka-lia
- ✓ panda-shuka
- ✓ babaika-tulia
- ✓ pokea-aga
- ✓ zama-elea
- ✓ vaa-vua

| **kitenzi** | **tendea** | **tendwa** | **tendewa** | **tendana** | **tendeka** | **tendeana** | **tendesha** | **tendeshea** | **tendesheka** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **cha**<br>✓ ogopa | chia | chwa | chiwa | chiana | chika | chiana | chisha | chishia | chishika |
| **cha**<br>✓ pambazuka | chea | 0 | chewa | 0 | 0 | 0 | chesha | cheshea | chesheka |
| **chwa**<br>✓ jua kuanza kutua | chwea | 0 | chwewa | chweka | 0 | 0 | chwesha | chweshea | chwesheka |
| **fa**<br>✓ tokwa na uhai | fia | 0 | fiwa | fika | 0 | fiana | fisha | fishia | fishika |
| **gwa**<br>✓ anguka | gwia | 0 | gwiwa | 0 | 0 | gwiana | gwisha | gwishia | gwishika |
| **ja**<br>✓ sogea karibu | jia | 0 | jiwa | jika | 0 | jiana | jisha | jishia | jishika |
| **la** | lia | liw | liwa | lika | lana | liana | lisha | lishia | lishika |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ✓ tia chakula kinywani na kumeza | | a | | | | | | | |
| **nya**<br>✓ enda haja kubwa<br>✓ anguka matone | nyea | nyewa | nyewa | nyeka | 0 | nyeana | nyesha | nyeshea | nyesheka |
| **nywa**<br>✓ tia kitu majimaji kinywani na kukimeza | nywea | nywewa | nywewa | nyweka | 0 | nyweana | nywesha | nyweshea | nywesheka |
| **pa**<br>✓ kabidhi | pea | 0 | pewa | peka | pana | peana | pesha | peshea | pesheka |
| **pwa**<br>✓ maji toka ufuoni hadi mbali ya bahari | pwea | 0 | pwewa | pweka | 0 | 0 | pwesha | pweshea | pwesheka |
| **ta**<br>✓ taga | tia | o | tiwa | tika | 0 | 0 | tisha | tishia | tishika |
| **wa**<br>✓ tokea | wia | 0 | wiwa | wika | wana | wiana | wisha | wishia | wishika |

**Matumizi ya Maneno na Viambishi Maalum**
**Maneno Maalum**

- **ila**

a) isipokuwa
✓ Watu wote **ila** yeye wameenda.
b) kasoro
✓ Hakuna kizuri kisicho na **ila**.

- **labda** (pengine/shaka)

✓ Haonekani siku hizi **labda** amepata uhamisho.

- **ikiwa**

a) (kama/shaka)
✓ Tutamkuta nyumbani **ikiwa** amepewa likizo.
b) masharti
✓ Mgonjwa atapona **ikiwa** atakunywa dawa ipasavyo.

- **walakini**

a) dosari
✓ Ghorofa limebomolewa kwa sababu lilikuwa na **walakini**.
b) lakini/bali
✓ Nimekula **walakini** sijashiba.

- **ingawa/ingawaje** (hata kama)

✓ Nilijilaza kitandani **ingawa** sikuwa na usingizi.

- **ijapokuwa/japo** (hata kama)

✓ Usicheze na nyoka **ijapokuwa** ni mdogo.

- **jinsi**

a) njia/utaratibu wa kufanyia jambo
✓ Sijui **jinsi** ugali unavyopikwa.
b) aina/namna/sampuli
✓ Siwezi kula chakula **jinsi** hii.
c) kulingana na/kama
✓ Alikuja **jinsi** alivyoniahidi.

- **kwa**

a) mahali
✓ Ameenda **kwa** Juma.
b) jinsi
✓ Alisoma **kwa** bidii.
c) sehemu ya kitu kisima/akisami
✓ Amepata alama moja kwa tano katika mtihani.
d) pamoja na
✓ Harusi ilihudhuliwa na wazee **kwa** vijana na tulikula wali **kwa** nyama.

e) kuonyesha kitu kilitumiwa kama kifaa
✓ Alikata mkate **kwa** kisu.
f) sababu
✓ Aliugua **kwa** kunywa maji machafu.
g) kuunganisha vipashio viwili
✓ Leo ndiwe utapika **kwa hivyo** tayarisha viazi.
h) muda/kipindi
✓ Alilia **kwa** nusu sana.
i) kufanya jambo bila kupoteza wakati
✓ Baada ya kula, tulienda moja **kwa** moja kulala.
j) kivumishi cha a-unganifu cha ngeli ya KU
✓ Kucheka **kwa** Maria kunaudhi.
k) umiliki wa mahali
✓ Twende nyumbani **kwangu**.

▪ **na**
a) kiunganishi
✓ Mama **na** baba wanalima.
b) umilikaji
✓ Kamau **ana** kitabu kizuri.
c) wakati uliopo
✓ A**na**andika barua.
d) kauli/mnyambuliko
✓ Kamau na Juma wanapiga**na**.
e) kuonyesha tofauti
✓ Kiatu hiki ni tofauti **na** kile.
f) mtenzi
✓ Alipigwa **na** mwalimu.
g) kuonyesha ufupisho wa nafsi
✓ Alisaidiwa **nao**.

**Zoezi**
a) Eleza matumizi ya na katika sentensi zifuatazo:
i) Baba **na** mama wa**na**piga**na** kwani a**na** tabia ya kulewa.
ii) Mtoto aliteswa **na** mama yake kwa kuwa tofauti na wengine **na**mi kikamkanya.

▪ **wala** (kukanusha)
✓ Sikumtusi **wala** kumpiga.

**Viambishi Maalum**

▪ **me/ja** (hali timilifu/kitendo kutendeka na si muda mrefu uliopia)
✓ Mama a**me**wasili.
✓ Mama ha**ja**wasili.

▪ **hu**
a) mazoea/jambo hutokea kila wakati
✓ Yeye **hu**lala mapema.
b) kikanushi
✓ **Hu**kutibiwa vizuri.

▪ **li**
a) wakati uliopita
✓ A**li**tupatia zawadi.
b) ngeli
✓ Tunda **li**meiva.
c) kitenzi kishirikishi kipungufu
✓ Jembe **li** ghalani.

▪ **ni**
a) nafsi ya kwanza umoja
✓ **Ni**liwasili jana.
b) mahali
✓ Twende kanisa**ni**.
c) kitenzi kishirikishi kipungufu
✓ Yeye **ni** daktari.
d) wingi
✓ Toke**ni** nje.

▪ **ndi-** (kitenzi kishirikishi kipungufu)
✓ Yeye ndiye aliniibia pesa.

▪ **ji**
a) udogo
✓ Ki**ji**tu kimeanguka.
b) ukubwa
✓ **Ji**bwa limebweka.
c) kirejeshi
✓ Ali**ji**palia makaa.
d) nafsi ya pili
✓ **Ji**chukulie upendacho.
e) kiambishi tamati cha kuunda nomino.
✓ Mwimba**ji** alituzwa.

▪ **Ki**
a) kitendo ki katika hali ya kuendelea
✓ Tulikuwa tu**ki**la alipoingia.
b) masharti/kitendo kinategemea kingine
✓ Utapita mtihani u**ki**jitahidi.
c) udogo
✓ Kitoto **kinalia**.
d) ngeli
✓ **Ki**tabu **ki**mechukuliwa.
e) kitenzi kishirikishi kipungufu
✓ chakula **ki** mezani.
f) kielezi namna mfanano.
✓ Yeye hula **ki**fisi.
g) kitendo hakifanyiki kamwe
✓ Chai hii hainywe**ki**.

▪ **ku**
a) kikanushi cha wakati uliopita
✓ Ha**ku**mpiga kwa jiwe.
b) nafsi ya pili umoja.
✓ Ali**ku**pigia simu jana.

c) mahali
✓ Hu**ku** **ku**mesafishwa.
d) ngeli
✓ **Ku**ugua **ku**memnyenyekesha.
e) mwanzo wa kitenzi
✓ Ameenda **ku**safisha nyumba.

- **ka**

a) mfuatano wa matukio
✓ Tulikula chakula, tu**ka**nywa chai kisha tu**ka**lala.
b) vichwa vya habari
✓ Mwizi **ka**pigwa mawe
c) kutoa amri
✓ **Ka**chezeeni nje!
d) kitendo fulani ni tokeo la kingine
✓ Tulisoma kwa bidii tu**ka**pita mtihani.
e) kutoa nasaha/shauri
✓ **Ka**mwombe babako msamaha.

- **a**

a) Hali isiyodhihirika ya wakati uliopo
✓ Watoto wacheza uwanjani.
b) vichwa vya habari
✓ Waziri **a**aibishwa na wananchi.
c) kitendo kinaendelea
✓ **Twa**enda sokoni.
d) nafsi ya tatu umoja
✓ Yeye **a**liudhika sana.
e) ngeli
✓ Mbuzi yule **a**tachinjwa kesho.
f) kiishio
✓ Mtoto amekul**a** vizuri.

- **nge/ngali** (masharti yanayowezekana au yasiyowezekana)

✓ Ningekuwa na pesa, ningenunua kiatu.
✓ Laiti ningalijua nisingaliingia katika hilo basi.

- **po**

a) wakati
i) maalum
✓ Yeye ana**po**lala hukoroma.
ii) Wowote/mazoea
✓ Mwalimu aingi**apo** wanafunzi husimama.
b) mahali
✓ Pali**po**safishwa pamechafuka.
c) masharti
✓ Mtoto aamka**po**, mpe uji.
d) kikanushi cha ki ya masharti
✓ Akila.-asi**po**kula.

Viakifishi

- **Alama za usemi("")**

a) Usemi halisi
✓ "Njoo kesho," mama akamwambia.
b) Lugha ngeni
✓ "Ninunulie jarida la 'Parents'", babake akamwambia.
c) Vipindi, filamu, makala
✓ "Vioja Mahakamani"
d) Semi
✓ "kumwaga zigo"

- **Dukuduku (…)**

a) maneno yameachwa ya kutangulia, kati au ya mwisho. Yaweza kuachwa kwa kuwa makali
✓ Nyani haoni…
b) kukatizwa usemi/kauli
AMINA: Mama ni…
MAMA: Kwanza watoka wapi usiku huu?
c) maneno yanaendelea
✓ Alimwambia ajihadhari anapovuka barabara…

- **Koma/mkato/kipumuo( , )**

a) pumziko fupi katika senyensi
✓ Tulipofika sokoni, tulinunua mboga.
b) kuorodhesha
✓ Alinunua mboga, samaki, nyanya na viazi.
c) kuonyesha mwanzo au mwisho wa usemi halisi
✓ "Njoo kesho,"mama akamwambia.
d) kuandika anwani
✓ Shule ya upili Gatwe, S.L.P 160, Kerugoya.
e) baada ya kutaja jina la mtu anayepewa habari
✓ Daktari, ningependa kukuona.
f) kutenganisha sentensi zenye masharti
✓ Usipofanya kazi, usile.
g) kuandika tarehe
✓ Alizaliwa mwezi wa Julai, tarehe 18, 1999.
h) kuandika tarakimu zinazozidi elfu
✓ 1,000, 13,000, n.k.

- **Ritifaa/kibainishi( ' )**

a) herufi imeachwa
✓ wal'otutuma
b) shadda/mkazo
✓ `iba, ka`lamu
c) katika sauti ya king'ong'o
✓ Ng`ombe amekufa.
d) Kufupisha
✓ Tu'shasafisha nguo.
e) katika kuandika miaka yenye namba izilizoachwa

- ✓ `73-`99.
- ▪ **Mshazari/mkwaju(/)**
- a) Tarehe
- ✓ Alizaliwa tarehe 5/6/1998.
- b) kuonyesha kumbukumbu
- ✓ KUMB 1/2009
- c) kuonyesha visawe
- ✓ Nenda katika shule/skuli.
- d) Kuonyesha au
- ✓ Wanawake/wanaume wataajiriwa.
- ▪ **Kistari kifupi( - )**
- a) kuandika tarehe
- ✓ 5/6/2006
- b) kuonyesha silabi, viambishi au mofimu
- ✓ sa-la-mu na imb-a.
- c) kuonyesha neno linaendelea katika mstari unaofuata.
- ✓ Usitenganishe sauti za silabi.
- d) Kuonyesha mzizi wa neno
- ✓ -ma,-bwa
- e) kuonyesha kudumishwa kwa sauti
- ✓ Lo-o-o-o!
- f) Hadi/ kipindi cha tukio fulani
- ✓ 1999-2008.
- g) Kutenganisha usemi na msemaji
- ✓ Huo ni upumbavu-Kibaki
- ▪ **Kistari kirefu(___)**
- a) kutenganisha usemi na msemaji
- b) kuonyesha mabadiliko ya ghafla
- ✓ Wanafaunzi ni wajinga-samahani, simaanishi wote.
- c) kutangulia maelezo ya ziada
- ✓ Walisaidia nchi za Afrika Mashariki-Kenya, Uganda na Tanzania kwa msaada
- ▪ **Mstari(¬¬ ___________)**
- a) kusisitiza
- ✓ Jibu maswali <u>mawili</u> pekee.
- b) kuonyesha aina za maneno
- ✓ Mtoto <u>wangu</u> analala (V. kimilikishi).
- c) kuonyesha vitabu, majarida na magazeti
- ✓ <u>Chemchemi za Kiswahili</u>, "<u>True Lo</u>ve", n.k.
- d) kuandika anwani/kichwa
- ✓ <u>Mwanafunzi Adhibiwa/Kaadhibiwa Vikali</u>
- ▪ **Kikomo/kitone/nukta (.)**
- a) mwishoni mwa sentensi.
- b) kuandika tarehe
- ✓ 2.3.2013
- c) kuonyesha ufupisho wa maneno
- ✓ Dkt.,Bw.,Bi.,C.C.M
- d) kuonyesha takwimu
- ✓ 4.5, 86.27, n.k.
- e) kutenga shilingi na senti
- ✓ 6.50-shilingi sita na senti hamsini
- f) juu ya herufi j na I
- ▪ **Nusu/semi koloni/nukta na kituo (:)**
- a) kugawa sentensi mbili zinazoweza kujisimamia bila ya viunganishi
- ✓ Wasichana walifuata maagizo waliyopewa; wafulana waliyagomea.
- b) kama kipumziko katika sentensi ndefu
- ✓ Alipochunguza ile hati aliyokabidhiwa na wale wafanya biashara aliona kuwa si nzuri; akaamua kujitenga nayo.
- ▪ **Vifungo/mabano/paradesi( )**
- a) kuzingira nambari au herufi katika orodha
- ✓ (i),(a)
- b) kuonyesha maelezo ya vitendo vya msemaji katika mazungumzo, mahojiano au tamthilia
- ✓ MAMA :( *Akiinama.*) Hebu njoo haraka.
- c) kutoa maelezo zaidi
- ✓ Ema (kifungua mimba changu) chaja leo kutoka marekani.
- d) kuonyesha visawe
- ✓ Mamba (ngwena) huliwa.
- ▪ **Herufi kubwa(H)**
- a) mwanzoni mwa sentensi.
- b) kuandika anwani
- ✓ S.L.P 1000, Bura.
- c) mwanzoni mwa usemi halisi
- ✓ "Twendeni zetu," akatwambia.
- d) baada ya kiulizi (?) na hisi (!)
- ✓ Lo! Ulienda? Hebu niambie yaliyojiri.
- e) mwanzoni mwa nomino za pekee
- ✓ Musa
- f) ufupisho wa maneno
- ✓ C.C.M (Chama cha Mapinduzi)
- g) mwanzoni mwa majina ya vitabu, majarida, magazeti, vipindi, filamu, n.k.
- h) kuandika sifa inayotokana na jina la pekee
- ✓ Kiganda, Kikristu.
- ▪ **Koloni/ Nukta mbili ( : )**
- a) kuorodhesha
- ✓ Ukitaka kuandaa samosa, unahitaji vitu hivi: unga, nyama, chumvi, mafuta na kitunguu
- b) kutangulia usemi halisi
- ✓ Alimwangalia kisha akamtupia: "mshenzi."
- c) kuandika mazungumo, mahojiano au

tamthilia
- ✓ MAMA :( *Akiinuka*.) Umechelewa wapi?

d) kutenganisha dakika na sekunde
- ✓ 9.25:05

e) kutangulia maelezo fulani
- ✓ Alipofungua mlango alishtuka: mizoga ya punda ilikuwa imetapakaa nje.

- **Hisi/mshangao (!)**

a) kuamrisha
- ✓ Kachezeeni nje!
- ✓ Kamau! Unafanya nini?

b) baada ya vihisishi
- ✓ Masalaale! Pesa zangu zote zimeibwa.

c) baada ya sentensi iliyo mshangao
- ✓ Gari langu limeibwa!

d) kusisitiza
- ✓ Kesho msichelewe kuwasili shuleni!

e) kudharau/kubeza
- ✓ Mwangalie! Kichwa kama jiwe.

f) baada ya tanakali
- ✓ Mate yalimdondoka ndo! Ndo! Ndo!

- **Kiulizo (?)**

a) mwishoni mwa sentensi iliyo swali

b) mwishoni mwa methali zenye muudo wa swali
- ✓ Pilipili usiyoila yakuwashiani?

c) kuonyesha shaka
- ✓ Kenyatta alizaliwa mwaka wa 1945(?)

d) kuonyesha mwaka wa kuchapishwa kwa kitabu haujulikani
- ✓ Mlacha J (?) Tujijue Ipasavyo

- **Herufi nzito (h)**

a) kusisitiza
- ✓ Jibu maswali *manne* pekee.

b) kuonyesha wakati/njeo au hali
- ✓ Nilicheza,Nimelima

c) kuonyesha umoja na wingi
- ✓ **m**toto-**wa**toto

d) kuonyesha aina ya neno katika sentensi
- ✓ Mtoto **wake** amelala (kivumishi)

- **Herufi za mlazo/italiki(*h*)**

a) kuonyesha aina ya kiambishi au mofimu
- ✓ Ki-li-*cho*-ib-w-a (kirejeshi).

b) kusisitiza
- ✓ Jibu maswali *mawili*.

c) kuonyesha jina la kitabu
- ✓ *Nyota ya Rehema*

d) kuonyesha maneno ya kigeni
- ✓ Napenda *mukimo.*

e) kuonyesha maelezo ya vitendo vya mhusika katika mazungumzo, mahojiano na tamthilia
- ✓ AMINA: (*Akiinuka)* Mama ameenda kwa Farashuu.

- **Kinyota(*)**

a) kuonyesha neno limeendelezwa vibaya
- ✓ *kitaabu

b) kuonyesha sentensi haina mpangilio sahihi wa maneno
- ✓ *Kisu cha hiki ni nani?

c) kuonyesha tanbihi (maelezo ya neno yanapatikana chini mwa ukurasa)
- ✓ idhibati*

d) kuonyesha sentensi ina makosa kisarufi
- ✓ *Kuku hii ni ya nani?

**Usemi Halisi**

⇒ Maneno halisi kama yanavyotamkwa na msemaji.

a) Huandikwa bila kugeuza chochote.

b) Huanzia kwa herufi kubwa.

c) Hunukuliwa kwa alama za usemi ambazo huandikwa zikiwa mbili mbili na moja moja katika dondoo ndogo k.m. “Mwambie ‘ugua pole’ ukimuona,” baba aliniambia.

d) Koma hutumiwa mwanzoni au mwishoni mwake.

e) Msemaji mpya anapoanza kusema, unapaswa kufungua aya mpya k.m.
Alimuuliza, “Huendi kwa nini?”
“Sikupewa ruhusa,” alijibu Zahara.

f) Baada ya (?) na (!) na (.) maneno huanzia kwa herufi kubwa k.m. Lo! Unatoka wapi saa hii? Aliniuliza.

**Usemi wa Taarifa**

⇒ Ripoti kuhusu mambo yaliyosemwa na mtu mwingine.

a) Si lazima maneno yatokee yalivyosemwa. Yanaweza kubadilishwa mradi ujumbe ubakie ule ule.

a) Alama za mtajo, kiulizi na hisi hazitumiki.

b) Maneno “kwamba’ na ‘kuwa’ hutumiwa.

c) Baadhi ya maneno na viambishi hubadilika k.m.

| usemi halisi | usemi wa taarifa |
|---|---|
| -angu | -ake |
| -etu | -ao |
| -enu | -ao |
| -ako | -ake |
| wiki ijayo | wiki iliyofuata |
| kesho | siku iliyofuata |
| leo | siku hiyo |
| sasa | wakati huo |
| huyu | huyo |
| hii | hiyo |
| ta/ki | nge |
| ni | a |
| na | li |
| jana | siku iliyotangulia |
| Lo! | alishangaa |
| ? | alitaka kujua |

**VITATE**
**T/D**
**Tata**
a) hali ya kutoeleweka
✓ sentensi hii ni **tata.**
b) fundo katika uzi
✓ uzi umeingia **tata/umetata.**
**Dada**
a) ndugu wa kike

**Tua**
b) shuka kutoka angani
✓ ndege ili**tua** uwanjani.
c) weka chini k.v. mzigo
**Dua**
a) maombi kwa Mungu
✓ omba **dua**
✓ piga **dua** –apiza/laani

**Toa**
a) ondoa kitu ndani ya kinginea
b) kinyume cha jumlisha
**Doa**
a) alama yenye rangi tofauti na mwili wa kitu
b) dosari/ila/walakini
**Ndoa**
a) arusi/makubaliano rasmi ya mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kama mke na mume/chuo

**Tundu**
b) uwazi mdogo wa mviringo kwenye kitu k.v. sindano
c) kitu maalum cha kuwekea ndege kilichotengenezwa kwa mabati, matete n.k.
**Dundu**
a) mdudu anayebeba uchafu
b) rundo la vitu /mtumba

**Tuma**
a) peleka kitu k.v. barua kwa njia ya posta
b) agiza mtu kufanya jambo
**Duma**
a) mnyama mkubwa mwenye umbo kama la paka
b) kamata, hasa katika vita

**K/G**
**Kuku**
a) aina ya ndege anayefugwa nyumbani
**Gugu**
a) mmea unaoota mahali usipotakiwa
b) mmea wa mwituni mfano wa unyasi

**Kuni**
a) vipande vya mti vya kukokea moto
**Guni**
a) shairi la arudhi lililokosa kutosheleza kanuni moja au zaidi ya uandishi

**Kuna**
b) kwaruza kwa kucha /kitu chenye menomeno
**Guna**

a) toa sauti ya kuonyesha kukataa, kutoridhika, au kuchukia jambo.

**Kenge**
a) mnyama kama mjusi mdogo
**Genge**
a) kundi la watu
b) pango/shimo

**Kesi**
a) daawa/mashtaka yanayosikilizwa mahakamani
**Gesi**
a) hewa inayotumiwa kupikia au kutiwa katika vinywaji
b) hewa ambayo haigeuki na kuwa majimaji katika joto la kawaida

**CH/J**
**Changa**
a) toa kitu ili kukusanya kwa kusudi fulani
b) siokomaa
c) chanja/pasua vipande vipande vidogo vidogo k.v. kuni
**Janga**
a) hatari/balaa

**Chema**
a) kizuri
**Jema**
a) zuri

**Chini**
a) kwenye ardhi/sakafu
**Jini**
a) shetani/ mtu muovu

**Choka**
a) pungukiwa na nguvu baada ya kufanya kazi
**Joka**
a) nyoka mkubwa sana

**Chungu**
a) chombo kinachofinyangwa cha kupikia
b) kinyume cha tamu
c) idadi kubwa (chungu nzima)
d) mdudu mdogo wa jamii ya siafu

**Chambo**
a) kinachowekwa kwenye mtego kunasia wanyama,samaki n.k.
**Jambo**
a) habari,tukio shughuli

**Kucha**
a) elekea asubuhi
b) ogopa
**Kuja**
a) hali ya kusogea karibu

**Chuma**
a) pata mali
b) madini magumu yanayotumiwa kujengea na kuundia vitu
c) tungua matunda au maua kutoka mtini
**Juma**
a) wiki
b) jina la mtu

**Chenga**
a) hepa kwa hila
b) mchele uliovunjikavunjika(mchele wa chenga)

**Jenga**
a) aka nyumba
b) fanya madhubuti/imarisha

**Mchi**
a) mti wa kupondea kwenye kinu
**Mji**
a) makazi ya watu wengi kulikojengwa nyumba nyingi
b) mahali kaburini anapowekwa mauti
c) sehemu ya kati ya chupa ya mwanamke mja mzito inayounganisha mtoto na mwili wa mama

**Kichana**
a) kitu cha kuchania nywele
**Kijana**
b) mtu wa makamo mwenye nguvu/mtoto wa kiume kabla ya kubaleghe

**F/V**
**Faa**
c) kusaidia
d) kuwa vizuri
**Vaa**
a) eneza kitu katika mwili ili kufunika sehemu fulani

**Fua**
a) safisha nguo
b) tengeneza kitu kutokana na madini

c) toa maji katika chombo
✓ **fua** maji
d) Haku**fua** dafu. (hakufaulu)
**Vua**
a) pata samaki kwa kutumia wavu, mshipi, ndoana n.k.
b) ondoa nguo mwilini
c) nusuru, okoa, ponya
d) **vua** macho (tazama)

**Fika**
a) wasili mahali
b) bila shaka/kabisa
**Vika**
a) valisha

**Fuka**
a) toa moshi bila kuwaka
b) uji wowote mwepesi (uji **fuka)**
**Vuka**
a) enda upande wa pili

**Fuma**
a) piga kwa mkuki
b) ona kwa ghafla bila kutazamia mtu anayetenda jambo ovu
c) tengeneza kitu kwa kusokota nyuzi,ukindu n.k
**Vuma**
a) julikana kwa watu wengi k.v. habari, mtu n.k.
b) toa sauti nzito k.v. simba,.upepo mkali,.ngoma n.k.

**Afya**
a) hali nzuri ya mwili/siha
**Avya**
b) toa mamba
c) tumia ovyoovyo mali, pesa, n.k.

**Fito**
a) vipande vya miti au chuma vya kujengea nyumba
**Vito**
b) mawe ya thamani

**Fuja**
a) tumia vibaya
b) haribu mali, nguo ,chakula n.k.
**Vuja**
a) pita kwa kitu mahali penye upenyo
✓ Gunia hili lina**vuja.**
**Vunja**
a) fanya kitu kigumu kuwa vipande vipande
b) badilisha pesa ziwe ndogondogo
c) enda kinyume na kanuni

**Futa**
a) pangusa
b) chomoa kisu
c) toa maji nje ya chombo/fua maji
**Vuta**
a) fanya kufuata/burura
b) ingiza hewa au moshi mapafuni

**Wafu**
a) waliokufa
**Wavu**
b) utando wa nyuzi wa kufulia samaki,kutegea wanyama,kuweka golini/kimiani n.k

**CH/SH**
**Chaka**
a) mahali penye miti iliyosongamana
b) msimu wa kaskasi/joto na ukavu wa ardhi
**Shaka**
a) wasiwasi
b) tuhumuma

**Chali**
a) lala mgongo juu kichwa chini
b) mtu anayechekesha watu kwa kuwatolea mkasa
**Shali**
a) kitambaa cha begani cha shehe
**Shari**
b) balaa (pata **shari)**

**Chati**
a) mchoro unaotoa maelezo Fulani
**Shati**
a) vazi la juu la mwili lenye mikono
**Sharti**
a) ¬lazima

**Choka**
a) pungukiwa na nguvu baada ya kufanya jambo kwa muda mrefu
**Shoka**
a) kifaa cha kukatia na kupasulia miti

**Chombo**
a) ala ya kufanyia kazi
**Shombo**

b) harufu mbaya ya samaki

**Chokoa**
a) tia kitu chenye ncha kwenye tundu au shimo ili kutoa kitu k.m **chokoa** meno
**Shokoa**
b) kazi ya kulazimishwa (fanyishwa **shokoa)**
c) shamba lililolimwa na kuachwa kumea nyasi

**TH /DH**
**Thamini**
a) tia maanani, heshimu
**Dhamini**
a) toa pesa maakamani ili mshtakiwa asitiwe korokoroni

**Thamani**
a) kima
**Dhamana**
a) malipo ya kortini

**Thibiti**
a) kuwa ya kweli/kuaminika
b) Habari ime**thibiti.**
**Dhibiti**
a) tia mkononi
b) Nikidhibiti pesa zangu kutoka kwake nitanunua baiskeli.
c) weka chini ya mamlaka

**Ridhi**
a) kubali
b) pendezwa na jambo
**Rithi**
a) miliki kitu kutoka kwa mtu aliyekufa ama uliye na uhusiano naye
b) pata jambo au ujuzi kutoka kwa mtu mwingine

A/H
**Apa**
a) tamka jina aghalabu la Mungu kuthibitisha jambo Fulani
**Hapa**
a) mahali karibu

**Ama**
a) au
**Hama**
toka mahali fulani ili kwenda mahali pengine kuishi (gura)

**Adimu**
a) -a shida kupatikana,nadra
**Hadimu**
a) -mtumishi (mahadimu)

**Ajali**
jambo la madhara au hatari
**Hajali**
a) kinyume cha jali

**Auni**
a) saidia
**Launi**
a) rangi

**L/R**
**Lahani**
a) tuni
**Rahani**
a) chumba maalum katika nyumba au chombo cha kuwekea vitu

**Lea**
a) tunza mtoto
**Rea**
a) ghadhibika

**Lemba**
a) nyanganya kwa hila,punja
**Remba**
a) pamba, rembesha
**Fahali**
a) ng`ombe dume
**Fahari**
a) -a kujivuniwa kwa watu

**Mahali**
a) sehemu ambapo mtu au kitu huweza kukaa
**Mahari**
a) mali au fedha inayotolewa na mwanamme kupewa wazazi wa mwanamke anayetaka kumuoa
**S /SH**
**Saba**
a) namba inayoonyesha idadi
**Shaba**
a) madini yenye rangi ya manjano

**Saka**
a) tafuta,winda
**Shaka**

a) wasiwasi
b) tuhuma
c) kutokuwa na hakika

**Suka**
a) tikisa kitu
b) pitisha kitu kama nywele baina ya zenyewe kupata mfumo fulani

**Shuka¬**
a) enda chini kutoka juu ya kitu
b) kitambaa cha kujifunga kiunoni

**Soga**
a) mazungumzo ya kupitisha wakati

**Shoga**
a) jina waitanalo wanawake marafiki
b) msenge

**Sababu**
a) kinachofanya jambo kutokea,chanzo

**Shababu**
a) kijana

**J/NJ**

**Jaa**
a) tosha
b) tapakaa kila mahali
c) mahali pa kutupia taka

**Njaa**
a) hali ya tumbo kutaka kupata chakula
b) ukosefu mkubwa wa chakula

**Chema**
a) kizuri

**Jema**
a) zuri

**Njema**
a) nzuri

**Jia**
a) sogelea karibu

**Njia**
a) barabara
b) namna au jinsi ya kufanya jambo

**Jozi**
a) vitu viwili vinavyofanana vilivyo pamoja

**Njozi**
a) maono yatokeayo usingizini;ruia

**Jana**
b) siku kabla ya leo,mwaka kabla ya huu
c) buu la nyuki-kama kiluwiwi cha nzi

**Njana**-samaki mwenye rangi nyekundu

**D/ND**

**Dege**
a) eropleni kubwa
b) ndege mkubwa
c) ugonjwa wa watoto unaosababishwa na homa kali

**Ndege**
a) mnyama aghalabu anayeruka kwa mabawa
b) eropleni inayosafiri angani
c) ndege mbaya/mzuri (bahati nzuri/mbaya)

**Duni**
a) kitu chenye thamani ya chini

**Nduni**
b) ajabu/lisilo la kawaida

**B/MB**

**Basi**
c) gari la abiria
d) kisha

**Mbasi**
rafiki

**Buni**
a) gundua
b) unda
c) tunga

**Mbuni**
a) ndege asiyeweza kuruka lakini huenda mbio sana
b) mkahawa au mti uzaao kahawa

**Bali**
a) lakini
b) sijali wala si**bali** (kusisitiza kutojali)

**Mbali**
a) si karibu
b) tofauti

**Mbari**
a) ukoo

**Bega**
a) sehemu ya mwili juu ya mkono na chini ya shingo

**Mbega**
a) nyani
b) manyoya ya ndege wanayojifunga wachezaji ngoma (jifunga **mbega)**

**Iba**

a) chukua kitu cha mtu mwingine bila ruhusa

**Imba**

b) tamka maneno kwa sauti ya mziki

**G/NG**

**Gawa**

a) tenga katika sehemu mbalimbali
b) aina ya ndege wa usiku;kirukanjia

**Ngawa**

a) mnyama afananaye na paka

**Guu**

a) mguu mkubwa sana

**Nguu**

a) kilele cha mlima
b) nguru_aina ya samaki

**Goma**

a) kataa kufanya jambo mpaka masharti fulani yatimizwe
b) ngoma kubwa sana
c) duwi (aina ya samaki)

**Ngoma**

a) ala ya mziki inayotengenezwa kwa kuwambwa ngozi kwenye mzinga (piga ngoma*)*
b) mchezo wa kufuata mdundo wa ngoma (cheza ngoma)

**Koma**

a) alama ya kituo
b) acha kufanya jambo

**P/B**

**Pata**

a) kuwa na jambo, hali au kitu
b) kuwa kali

✓ Kinolewacho hu**pata**.

**Bata**

ndege mwenye vidole vilivyotandwa aghalabu akaaye majini

**Papa**

samaki mkubwa

**Baba**

mzazi wa kiume

**Pana**

a) kinyume cha –embamba

**Bana**

finya

**Bango**

uwazi ulio ardhini,mtini au jabalini

**Bango**

kipande cha karatasi ngumu kama kadi

b) bati linalozuia matope juu ya gurudumu la gari au baiskeli

**Pacha**

a) watoto wanaozaliwa kutokana na mamba moja

**Bacha**

b) tundu kwenye ukuta; shubaka(*closet)*

**Paja**

a) sehemu ya mguu kati ya goti na nyonga

**Pania**

a) kazana ili kufanya jambo lililokusudiwa

**Bania**

a) zuia kitu bila ya kutaka kukitumia (bania pesa)

**Pima**

a) tafuta urefu, uzito n.k.

**Bima**

a) mkataba na shirika wa kulipa pesa ili kupata fidia mtu anapofikwa na hasara

**Punda**

a) mnyama

**Bunda**

a) fungu la karatasi,noti,ngozi n.k

**Panda**

a) enda juu
b) kifaa cha kurushia vijiwe; manati
c) baragumu
d) tia mbegu ardhini ili zimee

**Banda**

jengo kubwa la kuwekea vitu au wanyama

**Pasi**

a) fuzu/faulu
b) hati inayomruhusu mtu kusafiri nje ya nchi/pasipoti
c) chombo cha kunyooshea nguo

**Basi**

a) gari kubwa la abiria

**Mbasi**

b) rafiki

**T/D**

**Tamu**

a) enye ladha ya kuridhisha mdomo

**Damu**

a) maji mekundu yanayozunguka mwilini
b) ukoo

**Taka**

a) kuwa na haja ya jambo fulani
b) uchafu

**Daka**

a) pokea kwa mikono kilichorushwa
b) tunda bichi (nazi daka/danga)

**Tokeza**

a) fanya kuonekana

**Dokeza**

a) toa habari za siri kwa uchache

**Tai**

a) ndege mkubwa mwenye makucha marefu alaye mizoga (*vulture)*
b) kitambaa kinachovaliwa kwenye ukosi wa shati

**Dai**

*a)* taka kupewa kilicho chako
*b)* habari inayosemwa na haijathibitishwa

**K/G**

**Kamba**

a) uzi mnene
b) samaki mdogo
c) mnyama wa baharini mwenye miguu mingi ambaye huliwa
d) kata kamba (kimbia)

**Gamba**

a) ngozi kama pembe ya kasa, samaki ,kasa au kobe(*scales)*

**Konga**

a) kuwa mzee
b) kusanya vitu au watu mahali pamoja (kongamano)
c) meza maji kidogo ili kupunguza kiu (konga roho)

**Gonga**

kutanisha kitu kimoja na kingine kwa kuvipiganisha

**Koti**

vazi zito livaliwalo juu ya nguo

**Korti**

mahakama

**Goti**

kiungo cha mguu kinachounganisha paja na muundi

**Mfugo**

mnyama anayefugwa nyumbani kwa ajili ya kuliwa au biashara

**Mfuko**

kitu cha kitambaa cha kutilia vitu

**Tegua**

a) fanya mtego usifanye kazi
b) ondoa chombo kama chungu mekoni
c) fanya kiungo cha mwili kifyatuke

**Tekua**

a) angusha kwa kusukuma
b) ng`oa kwa nguvu k.v. mmea

**Mkuu**

kiongozi
wenye hadhi kubwa

**Mguu**

kiungo cha binadamu au mnyama cha kusimamia au kutembelea

**Oka**

tia ndani ya tanuu kitu ili kiive au kikauke k.v unga uliokandwa au matofali

**Oga**

a) safisha mwili
b) enye hofu

**Pika**

a) weka kitu k.v. chakula sufuriani juu ya moto ili kiive

**Piga**

a) kutanisha vitu kwa nguvu
b) piga chafya, maji, hodi n.k.

**Ukali**

a) hali ya kutokuwa mpole
b) hali ya uchungu (ladha)

**Ugali**

a) chakula kinachopikwa kwa unga wa mahindi na kusongwa na maji moto hadi yakauke